



**SWAHILI A1 – HIGHER LEVEL – PAPER 2**  
**SOUAHÉLI A1 – NIVEAU SUPÉRIEUR – ÉPREUVE 2**  
**SWAHILI A1 – NIVEL SUPERIOR – PRUEBA 2**

Tuesday 11 May 2004 (morning)

Mardi 11 mai 2004 (matin)

Martes 11 de mayo de 2004 (mañana)

2 hours / 2 heures / 2 horas

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works, will not score high marks.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- Ne pas ouvrir cette épreuve avant d'y être autorisé.
- Traiter un sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2<sup>e</sup> partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie n'obtiendront pas une note élevée.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.

*Andika insha kujibu moja ya msuala yafwatayo. Jibu lako lazima liwe juu ya angalau kazi mbili za sehemu ya 3 ulizojitayarisha nazo. Lazima uingize katika jibu lako mjadala wa kazi ya sehemu ya 2 ya utanzu mmoja kama inavyohusika. Majibu ambayo hayaegemei mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 hayatapata alama za juu.*

## **Tamthilia**

### **1. Ama**

- (a) “Tamthilia ya Kiswahili bado imo katika kuegemea kanuni za jukwaa na matini zenyewe kufuata kanuni za ‘Aristotle’ - hasa juu ya mtiririko wa hadithi kuanzia *mwanzo*, kupitia *kati* na na kumalizia *upeo*.” Je, unakubaliana na kauli hii? Jadili huku ukitoa mifano kutokana na angalau tamthilia mbili ulizosoma.

*Au*

- (b) Huku ukitoa mifano kutokana na angalau tamthilia mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, linganisha tamthilia mbili baina ya ile ilioandikwa kwa uwazi na ile iliyofumbwa kwa ishara.

## **Riwaya**

### **2. Ama**

- (a) “Kulingana na wana-tamthilia na washairi, mwandishi wa riwaya ana nafasi ya kujifaragua zaidi kwenye upana wa kujieleza na kuingiza kwenye riwaya yenye kila kitu na kila utanzu.” Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano kutokana na angalu kazi mbili ulizojitayarisha nazo.

*Au*

- (b) Waliganishe waandishi wawili wa riwaya angalau mbili ulizojitayarisha nazo kuhusu falsafa zao za maisha.

## **Ushairi**

### **3. Ama**

- (a) “Picha ni kipengele muhimu sana katika ushairi.” Huku ukitoa mifano mbalimbali kutoka angalau diwani mbili ulizojitayarisha nazo onyesha vipi picha zinatumwiwa na kwa taathira gani katika kazi zao.

*Au*

- (b) Ukitumia mifano kutokana na diwani mbili za mashairi ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, elezea ‘umuhimu’ wa marudiorudio ya sauti, maneno na fikra katika ushairi.

## **Riwaya ya Mapenzi**

### **4. Ama**

- (a) “Mapenzi yana ‘migogoro’ yake.” Kwa kutumia riwaya mbili za mapenzi ulizojitayarisha nazo, jadili migogoro inayojitokeza ndani ya riwaya hizo.

*Au*

- (b) “Riwaya ya kimapenzi huandikwa kwa lugha ya kimapenzimapenzi.” Huku ukitoa mifano kutoka angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, elezea unaifahamu vipi kauli hii na onyesha lugha ya mapenzimapenzi ikoje.

## **Masuala ya Ujumla**

### **5. Ama**

- (a) “Sanaa huitofautisha kazi ya fasihi na maandishi mengine yoyote.” Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano kutoka katika angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo.

*Au*

- (b) “Kazi moja ya mwandishi wa kazi ya fasihi ni kufurahisha wasomaji wake, ingawa wakati huohuo huweza kushawishi, kuelimisha, kuonya n.k.” Wajadili waandishi wawili wa kazi mbili za fasihi ulizozisoma uonyeshe vipi wanatekeleza kazi muhimu ya fasihi ya kuburudisha huku wakati huohuo wakishawishi, kuelimisha na kuonya.

*Au*

- (c) “Sifa moja ya kazi ya ushairi ni kwamba huwa inasimamia maana mbalimbali tofauti.” Katika angalau mashairi mawili ya waandishi tofauti uliyoyasoma onyesha jinsi mashairi hayo yanavyoibua maana mbalimbali tofauti.

*Au*

- (d) Katika angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo jadili wazo, la kwamba wahusika si lazima wawe wameumbwa ‘kikweli’ au ‘kimviringo’; wanaweza kuwa vivuli tu vya mawazo ya mwandishi.